# Profesa Mkenda asisitiza ubora elimu ya juu Afrika

**Na FURAHA OMARY**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, ameusisitiza Mtandao wa Wathibiti Ubora wa Elimu ya Juu Barani Afrika (AfriQAN), kuendelea kuimarisha ubora katika vyuo vikuu na kutokubali kuushusha kwa namna yoyote.

Pia, amesisitiza umuhimu wa vyuo vikuu barani Afrika kuendeleza ushirikiano zaidi kwa sababu vinapishana katika maeneo kadhaa.

Profesa Mkenda alisema hayo jijini Dar es Salaam, jana alipofungua mkutano wa 14 wa AfriQAN unaofanyika nchini kwa mara ya kwanza ukizishirikisha nchi 22.

Washiriki wa mkutano huo wa siku tatu ulioandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwa kushirikiana na mtandao huo ni wakuu wa taasisi za udhibiti ubora wa elimu ya juu, makamu wakuu wa vyuo vikuu, wakuu wa taasisi za elimu ya juu, jumuiya na asasi za kimataifa na kikanda, wanataaluma, mabaraza na bodi za wasajili wa watalaamu.

"Nimepata fursa ya kuzungumza na washiriki wa mkutano, lakini masuala makubwa ni kusisitiza bado tuendelee kuimarisha ubora katika vyuo vikuu na tusikubali kushusha ubora kwa namna yoyote.

"Shinikizo la kushusha ubora siku zote lipo, lakini lazima sisi tuhakikishe hatutofautiani na nchi nyingine yoyote duniani," alisema.

Profesa Mkenda alieleza maeneo muhimu ya washiriki hao kuyajadili likimemo uendeshaji wa vyuo vikuu ni biashara yenye ushindani mkubwa, hivyo katika ufundishaji wake kazi kubwa ni kuhakikisha vinawasaidia wanafunzi kufanya vizuri, inaposhindikana kabisa inabidi wanafunzi waache kusoma.

"Kwa mfano mtu anaposomea udaktari akionekana hawezi kumudu kabisa yale masomo, inabidi aondoke baadaye asiye kuwaumiza watu atakapokuwa daktari.

"Katika ushindani kusiwe kukawa na wazo kwamba kila kitu ni ada, hata kama hasomi chochote, tumwache tu akae chuo kikuu ama kuhakikisha wanatoa ufaulu mkubwa kuwavutia wanafunzi kuona chuo chako ni rahisi sana kufaulu vizuri," alisema.

Akizungumzia suala la kuajiri wahadhiri, Profesa Mkenda alibainisha kuna vigezo vya kufanya mtu awe mhadhiri, mhadhiri mwandamizi au profesa mshiriki au profesa, hivyo katika ushindani wa biashara kusiwe na presha ya kushusha viwango, kwa kuonesha chuo kina maprofesa wa kutosha.

Waziri huyo alisema viwango lazima viwe vya kimataifa, suala ambalo siyo kwa nchini tu, bali Afrika nzima.

Kuhusu kuongezeka idadi ya wanafunzi vyuo vikuu huku kukiwa na changamoto ya ajira, Profesa Mkenda alisema kuna suala la vyuo vikuu kupimwa jinsi gani vinamwandaa mwanafunzi kujiajiri na kuajirika kirahisi.

"Pamoja na hilo, lazima tuangalie hatushushi uwezo wa wanafunzi kufikiri kwa kuwa ukifanya hivyo watakuwa wameenda kusoma tu mambo ya ufundi, chuo kikuu kinapaswa kumfanya wanafunzi awe na uwezo wa kufikiri.

Mbali na hayo, Waziri Mkenda alivitaka vyuo vikuu barani Afrika kushirikiana huku akiahidi hapa nchini watajitahidi kuhakikisha vyuo hivyo vinashirikiana.

"Hapa nchini tutajitahidi kuvifanya vyuo vishirikiane, wakati mwingine unaweza kuwa na mhadhiri mzuri yupo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), akatoa mhadhara wake katika vyuo vingine kwa makubaliano maalumu.

"Sisi Butiama kile Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere tumeanza kuchukua wanafunzi kwa sababu ya ushirikiano kati ya kile chuo na Chuo cha Sokoine na UDSM kuhakikisha wanabadilishana wahadhiri, wanafunzi wanaenda wanasoma," alisema.

"Kuna umuhimu wa kushirikiana kuongeza ushirikiano wa vyuo vikuu vya Tanzania, lakini vya Afrika ni muhimu zaidi kushirikiana kwa sababu tunapishana katika maeneo kadhaa," alisema.

### TAFITI

Waziri Mkenda alisema chuo kikuu kazi yake siyo tu kurithisha uelewa, bali kuzalisha uelewa mpya na kufanya utafiti.

Alieleza utafiti kwa chuo kikuu ni jambo muhimu kwa kuwa hauwezi kuwa profesa kwa kutoa mhadhara tu, lazima uwe unafanya tafiti.

Profesa Mkenda alisema lazima vyuo vishirikiane kufanya tafiti kutatua matatizo ya wananchi kwa kuwa chuo kikuu ni taasisi ya utafiti na kufundisha.

Aliongeza vyuo vikuu vinapaswa kuendeleza na kuhimiza tafiti na kupongeza idadi ya wanafunzi, wahakikishe hawapunguzi muda wa wahadhiri kufanya tafiti na kusisitiza matumizi ya teknolojia katika ufundishaji.

### PROFESA KIHAMPA

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa TCU, Profesa Charles Kihampa alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kufungua milango, ambapo hivi sasa wanaweza kufanya mikutano mingi mikubwa.

"Huu ni mkutano mkubwa wa mtandao wa wadhibiti ubora wa elimu ya juu barani Afrika. Mtandao huu ulianzishwa mwaka 2009 na ni kwa mara ya kwanza mkutano unafanyika nchini," alisema.

Kwa mujibu wa Profesa Kihampa, huo ni mkutano wa 14 wa mtandao huo kwa kuwa ulikuwa ukifanyika nchi mbalimbali na Tanzania imekuwa ikihudhuria kwa kuwa ni muhimu, kwani inashirikiana na wadhibiti ubora kuanzia elimu ya msingi hadi ya juu.

"Kuna taasisi za kutoka nchi 22 barani Afrika na nchi tatu kutoka nje ya bara la Afrika ambazo tunashirikiana katika kuandaa utaratibu wa uendeshaji wa taasisi hususan za elimu ya juu. Hii ina manufaa elimu hususan ya juu, siyo ya nchini kwako pekee, bali unamtoa mhitimu anayeweza kuajirika ndani na nje ya nchi yako," alibainisha.

Profesa Kihampa alisema kupitia mtandao huo kuna vigezo vya udhibiti ubora walivyokubaliana vikiwemo sifa za mwalimu ziweje, mhitimu, elimu ya eneo fulani ambavyo vinasaidia wahitimu kupata ajira sehemu yoyote duniani.

"Unaweza kuwa na mtandao mdogo wa kikanda na ule mkubwa, wakati unaanzishwa kulikuwa na nchi 22 sasa zipo nyingi na Tanzania ni miongoni mwa waanzilishi kwa kuwa wazo la kuuanzisha lilianzia Dodoma. Makubaliano yalifikiwa Accra, Ghana, tunajisikia fahari mataifa zaidi ya 22 kuja nchini kujadili kuhusu ubora wa elimu ya juu," aliongeza.